

Mradi wa mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa Wilayani Monduli

Mradi wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi ni mradi ulipangwa kutekelezwa kwa miaka 5 amabo umelenga katika kugharimia vipaumbele vya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi Wilayani vilivyoibuliwa na wanajamii wa Monduli.

Mradi unatekelezwa katika Wilaya 3 za Monduli, Longido na Ngorongoro na pia mafanikio ya mradi huu katika Wilaya hizi 3 utasababisha kupanuka kwa mradi hadi Wilaya nyingine 12 za Tanzania.

- Mradi huu utasaidia Wilaya na mipango ya Wilaya kuweza kusaidia jamii kukabiliana na majanga yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na kusaidia kuinua shughuli za uzalishaji mali.
- Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID) pamoja na Taasisi ya kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED).
- Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ina mamlaka ya kulisimamia rasilimali za mradi kwa kushirikiana na shirika la Haki kazi catalyst na Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF).

Mradi wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi utekelezaji wake upo katika awamu 2.

Awamu ya kwanza imefanya yafuatayo;

- Kujenga uwezo katika ngazi ya Wilaya na jamii ambapo wataalam wa halmashauri walijengewa uwezo katika masuala mbalimbali ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na athari zake.
- Wilaya kwa kushirikiana na Hakikazi Catalyst waliwezesha jamii kuunda kamati za usimamizi wa mradi (**DIVISIONAL ADAPTATION PLANNING COMMITTEE**)
- Kamati hizi ndio zilizowezesha kusimamia mchakato mzima wa kuibua miradi ya mabadiliko ya tabianchi kutoka ngazi ya jamii hadi Tarafa.
- Pia katika awamu hii wilaya kwa kushirikiana na wanajamii pamoja na shirika la IIED/Haki kazi catalyst walitengeneza ramani za rasilimali za Wilaya “Resource Mapping” ambazo zinawezesha utambuzi wa rasilimali za Wilaya.
- Kuandaa taarifa ya ustahimilivu wa majanga yatonayo na mabadiliko ya hali ya hewa Wilayani Monduli “Resilience Assessment”

- Kwa kushirikiana na shirika la Tanzania Meteorological Agency (TMA) zimeundwa kamati za utabiri wa kijadi (Indigenous Knowledge) ili kuweza kupata tabiri za kijadi na kuzilinganisha na zile za kisasa.
- Kujenga uwezo kwa wanakamati za usimamizi wa mradi katika masuala mbali mbali ya usimamizi wa mradi.


Awamu ya pili:

Katika awamu hii utekelezaji unategemea kufanyika kwa mambo yafuatayo;

- Kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wanajamii ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.
- Kujenga uwezo wa wilaya katika kusimamia mradi na kuhakikisha mipango ya Wilaya inajumuisha mambo ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi(Institutional Capacity building).
- Kufanya sauti ya wanawake isikike kwa kuwashirikisha katika shughuli mbali mbali za maendeleo ambapo wakinamama wamekuwa wakijengewa uwezo katika mambo mbali mbali katika masuala ya utawala bora,mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi mfano baraza la wakina mama wa kifugaji Monduli(**BAWAKIMO**).

MUUNDO WA MRADI HUU TOKA NGAZI ZA JAMII

MUUNDO WA KAMATI YA MABADILIKO YA TABIANCHI NA HALI YA HEWA



**KAZI ZILIZOFANYIKA WILAYANI MONDULI KUANZIA MWEZI
JANUARI 2017**



**WANAJAMII WA KIJJI CHA MAJENGO WAKIWA KATIKA MCHAKATO
WA KUIBUA MIRADI YA JAMII.**



**KAMATI ZA KITARAFU ZIKIFANYA KAZI ZA VIKUNDI EG.
KUCHORA NADHARIA YA MABADILIKO (THEORIES OF
CHANGE) MTO WA MBU.**



KAMATI YA MRADI MANYARA IKIWA KATIKA MCHAKATO WA KUPITISHA MIRADI YA KITARAFU



KAMATI TARAFU YA KISONGO WAKIPITISHA MIRADI YAKITARAFU



WATAALAM WA HALMASAHURI NA HAKI KAZI CATALYST WAKIFANYA MREJESHO WA MAFUNZO MTO WA MBU.



AFISA MIPANGO (W) WA KWANZA KULIA NDUGU GODFREY LUGUMA PAMOJA NA MRATIBU WA MRADI (W) NDUGU JOSEPH RUTA WAKIWA KATIKA KIKAO CHA KAMATI YA WATAALAM NGAZI YA WILAYA KUPITIA MIRADI YA TARAFU.



KAMATI YA WILAYA YA MRADI PAMOJA NA WAWAKILISHI WA TARAFWA WAKIPITIA MIRADI KUTOKA TARAFWA

Katika kupitia miradi ngazi ya Wilaya, wawakilishi ngazi ya tarafa walikaribishwa kuja kushiriki mchakato huu. Kamati ya Wilaya ilijumuisha wakuu wa idara za Fedha, mipango, Kilimo, Mifugo, Ardhi maliasili na Mazingira pamoja, Misitu na maendeleo ya jamii.

Katika kikao hiki pia kulikuwa na mwakilishi kutoka Shirika la Haki kazi Catalyst amabae alishuhudia mchakato mzima na kutoa ushauri pale palipo hitajika.



WATAALAM WA HALMASHAURI WAKIWA NA WATAALAM KUTOKA CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA(LGTI) WAKIANDIKO ANDIKO LA MIRADI.

Wilaya iliandaa wataalam wa kuandika andiko ambao waliashirikiana na wawakilishi kutoka tarafa zote 3 na pia Wilaya ilitembelewa na wataalam kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI).

Uandikaji wa maandiko ulikuwa shirikishi kwa maana baada ya maandiko kuwa yameandikwa uwasilishwaji kwa njia ya “Power Point ulifanyika ili urekebishwaji wa pamoja ufanyike.



MKUU WA WILAYA NA MKURUGENZI MONDULI WAKIWA KATIKA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI YA WILAYA (ADVISORY BOARD) WAKIPTIA MIRADI ILIYOPITIWA NA KAMATI YA WATAALAM WILAYA.

KAZI ZINAZOFANYIKA KIPINDI HIKI :

Kitengo cha manunuzi kinakamilisha taratibu za manunuzi ambapo kuna miradi ambayo kazi zake zitaanza mapema kwa kuwa zitakuwa si za kutangaza bali ni kutafuta supplier wa kufanya kazi hizi ambapo jamii itashiriki kufanya kazi za mikono kama mradi miradi ya;

- Mradi wa kupunguza athari za mafuriko eneo la Mto wa Mbu
- Mradi wa kuweka vifaa vya hali ya hewa

Hizi zote zitatekelezwa baada ya Baraza kuwa limebariki mchakato mzima.

**Imeandaliwa na
Joseph A.Rutabingwa
Mratibu waMratibu
MONDULI**